SEHEMU YA KWANZA :LUGHA

# SHUGHULI ZA KISWAHILI

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 30.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako* *(iii). Nambari ya Knec*

***Muda:Saa 1 Dak 40***

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali la 1 hadi la 5.**

***(Liam anazungumza na mwalimu wake majilisini )***



**Liam** : Shikamoo mwalimu?

**Bi. Salama** : Marahaba Liam. Habari ya nyumbani?

**Liam** : Salama, tunashukuru Mola.

**Bi. Salama** : Mama anaendeleaje? Tulipata habari kuwa alijifungua.

**Liam** : Anapata nafuu. Alijifungua pacha.

**Bi. Salama** : Aha! Hongera kwake.

**Liam** : Shukrani. Nitamfahamisha mama.

**Bi. Salama** : Itakubidi utafute usaidizi kwa wenzako kufidia masomo waliyosoma ukiwa nyumbani ili uwe sawa nao.

**Bi. Salama** : Haya nenda darasani

**Liam** : Asante sana. Siku njema mwalimu.

**Bi. Salama** : Nawe pia

**1.** **"Shikamoo"** ni salamu za
   A. jioni pekee
   B. shuleni baina ya walimu na wanafunzi
   C. wadogo kwa walio na umri mkubwa
   D. wanafunzi kwa walimu pekee

**2.** Mazungumzo haya yanafanyika wapi?
   A. Majilisini
   B. Uwanjani
   C. Darasani
   D. Nyumbani

**3.** Ni neno lipi linadhihirisha kushangaa kwa Bi. Salama?
   A. Marahaba B. Nawe pia
   C. Habari za nyumbani D. Aha!

**4.** Kati ya majina haya, lipi si kisawe cha Mola?
   A. Maulana
   B. Stahimili
   C. Jalali
   D. Rabuka

**5.** Kutokana na mazungumzo haya, kuna uwezekano kuwa Liam
   A. alikuwa amezaliwa na pacha wake
   B. alikuwa mgonjwa
   C. alikosa vipindi fulani vya masomo
   D. alitaka kupewa nafasi akapumzike

**Soma makala haya kisha ujibu swali la 6 hadi la 10.**

Siku hizi, ajali za barabara zimekuwa nyingi kupindukia. Watu wengi wamepoteza maisha yao. Wengine wameachwa wakiwa na majeraha yaliyosababisha ulemavu. Imebainika kwamba, madereva wengi huendesha magari kwa kasi bila kuzingatia sheria za barabarani.

Madereva wengine huendesha magari yao wakiwa wamelewa chakari. Askari wa trafiki nao wanalaumiwa kwa kulegeza kamba. Baadhi ya askari hao, huchukua hongo barabarani kwa hivyo, hukosa kuchukulia hatua madereva waovu.

Ningependa kuomba serikali ipige msasa jambo hilo ili kukomesha maafa ya watu barabarani. Maderava wasiozingatia sheria za usafiri barabarani watiwe mbaroni. Askari wa trafiki wanaokubali kuhongwa nao vile vile wakamatwe na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

**6.** Ajali za wapi zimekuwa nyingi kupindukia?
A. Barabarani B. Hewani
C. Majini D. Sokoni

**7.** Askari gani wanaolaumiwa kwa kuchukua hongo?
A. Wa gereza B. Wa upelelezi
C. Hatujaelezwa D. Wa trafiki

**8.** Madereva wasiozingatia sheria za usafiri barabarani wafanyiwe nini?
A. Wapewe zawadi B. Watiwe mbaroni
C. Wasishikwe D. Wabembelezwe

**9.** Madereva wengine huendesha magari yao wakiwa
A. wamebeba sana
B. wamenenepa sana
C. wamelewa chakari
D. wameshiba sana

**10.** Ni lipi halisababishwi na ajali za barabarani?
A. Njaa
B. Ulemavu
C. Vifo
D. Majeraha

**Soma makala haya kisha ujibu swali la 11 hadi la 15.**

Baraka ni mwanafunzi mcha Mungu sana. Daima hakosi kujumuika na wenziwe pamoja na wavyele wake kwenda maabadini kusali.

Atokapo kusali, yeye husaidia kufanya kazi za nyumbani kama vile kufagia, kupanga vitabu, kusafisha vyombo na kunyunyizia maua maji. Aidha Baraka hutunza afya yake kwa kuoga, kupiga mswaki, kukata kucha na kuvaa nguo safi.

Mwalimu wa darasa anampenda Baraka kwa kudumisha usafi wake. Mwalimu humshauri Baraka pamoja na wanafunzi wenzake wale vyakula vya afya. Baadhi ya vyakula hivi ni ugali, mboga, samaki, uyoga,nyama, maharagwe na matunda yenye vitamini, kama vile mapera, machungwa, ndizi, maembe, matomoko, zabibu, karakara, mapapai na maparachichi.

Wanafunzi pia huhimizwa na mwalimu wao kulinda mazingira yao ili kuepuka magonjwa.

**11.** Baraka ni mwanafunzi wa aina gani?
A. Anayemchukia Mungu
B. Anayemdharau Mungu
C. Anayemchagua Mungu
D. Anayemheshimu Mungu

**12.** Baraka hujumuika na wenziwe kwenda wapi?
A. Kutembea kanisani
B. Kusali
C. Shuleni
D. Nyumbani

**13.** Maabadini ni mahali pa
A. mabati B. starehe
C. ibada D. karamu

**14.** Matunda humwongezea mtu nini mwilini?
A. Nguvu
B. Vitamini
C. Protini
D. Maji

**15.** Mazingira machafu huweza kusababisha
A. mvua nyingi B. kiangazi
C. njaa D. magonjwa



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16-20. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Shindano la upishi ___16____ shuleni ___17____. Wanafunzi kadhaa ___18____ na kushiriki. Kila mshiriki alipatiwa ___19___ vya mapishi kama vile chumvi, bizari, pilipili manga na vingine vingi. Majaji walikuwa na wakati mgumu kupata mshindi kwa kuwa wengi walitia ___20____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | A. iliandaliwa | B. waliandaliwa | C. yaliandaliwa | D. liliandaliwa |
| **17.** | A. yetu | B. mwetu | C. zetu | D. chetu |
| **18.** | A. walijitokeza | B. walitokeleza | C. walitokezwa | D. walijitosheleza |
| **19.** | A. viwango | B. bidhaa | C. viungo | D. vifua |
| **20.** | A. fola | B. fora | C. bora | D. dole |

**Kutoka swali la 21 hadi la 30, chagua jibu lifaalo zaidi kulingana na maagizo uliyopewa.**

**21. Tegua kitendawili:**
Popo mbili zavuka mto
A. Kufuli
B. Nywele
C. Barabara
D. Macho

**22.** Chagua nomino ya makundi isiyofaa
A. Mtungo wa samaki
B. Safu ya milima
C. Pakacha la watoto
D. Msitu wa miti


**23. Kamilisha methali ifuatayo**
Mpanda ngazi
A. hushuka
B. huchoka
C. ni fundi
D. husimama

**24.** Andika tarakimu 10002 kwa maneno
A. Elfu kumi na mbili
B. Kumi elfu na mbili
C. Elfu mbili na kumi
D. Kumi na mbili elfu

**25. Kanusha sentensi hii**
Nitamwambia anionyeshe njia
A. Nitamwambia asinionyeshe njia
B. Sitamwambia asinionyeshe njia
C. Sitamwambia anionyeshe njia
D. Nitamwambia asinionyeshe njia

**26.** Andika kwa udogo
**Mkono unauma**
A. Jikono linauma
B. kimkono kinauma
C. Kikono inauma
D. Kikono kinauma

**27.** Umbo hili huitwaje



A. Duara B. Mstatili
C. Mraba D. Pia

**28.** Andika kwa wingi
**Nitakununulia kitabu**
A. Tutawanunulia vitabu
B. Tutanunua vitabu
C. Tutakununulia vitabu
D. Tutamnunulia vitabu

**29.** Nitamwitaje mamake mama yangu?
A. Shangazi
B. Nyanya
C. Halati
D. Binamu

**30.** Bunda ni kwa noti kama vile biwi ni kwa
A. moshi B. pesa
C. taka D. maua



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## SEHEMU YA B: INSHA

| JINA LAKO | |
|---|---|

**Andika insha ya kusisimua kuhusu:-**

# UMUHIMU WA KILIMO



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com